

MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 SEPTEMBER, 2017) NA MATARAJIO YA MVUA KWA SIKU KUMI (11 – 200 SEPTEMBER, 2017)

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 SEPTEMBER, 2017)

Katika siku kumi za tatu za mwezi Agosti 2017, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo Kusini mwa Dunia (ST. Helena na Mascarene) ilianza kudhoofika na hivyo kudhoofisha mkondo wa mgandamizo mkubwa wa hewa wa Afrika Mashariki. Wakati ile migandamizo iliyopo sehemu ya Kaskazini ya dunia (Azores na Siberia) nayo pia ilianza kuimarika, hivyo kuruhusu ukanda wa mvua wa ITCZ kushuka kuelekea kusini . Joto la juu kidogo ya Wastani mpaka wastani liliendelea katika eneo la Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi. Kwa upande mwingine joto la bahari la chini ya wastani hadi wastani lilipimwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) Hali hii ilipelekea hali ya ukavu kwa maeneo ya magharibi mwa nchi na yale yaliyopo katika ukanda wa ziwa Victoria.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01–10 SEPTEMBER, 2017)

Mwenendo wa viashiria hapo juu vilipelekea hali ya ukavu katika maeneo mengi ya nchi, Hata hivyo vipindi vifupi vya mvua nyepesi viliendelea kuwepo katika maeneo ya mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza, Geita, Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Visiwa vya Unguja na Pemba. Hali ya ubaridi na vipindi vya upepo mkali viliweza jitokeza kutokana na kuendelea kuimarika kwa migandamizo ya hewa katika eneo la kusini mwa bara la Africa.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KATIKA SIKU KUMI (11 – 20 SEPTEMBER, 2017)

2.1 VIASHIRIA NA MFUMO WA MVUA KWA SIKU KUMI (01 – 10 SEPTEMBER, 2017)

Katika siku kumi za kati za mwezi September 2017, migandamizo mikubwa ya hewa iliyo Kusini mwa Dunia (ST. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika na hivyo kudhoofisha mkondo wa hewa wa Afrika Mashariki. Wakati, ile migandamizo iliyopo sehemu za Kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika na hivyo kuruhusu ukanda wa mvua wa ITCZ kuanza kushuka katika eneo uliyopo na kuelekea sehemu ya Kusini mwa Dunia. Joto la bahari la juu ya Wastani hadi wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi na hii inatarajiwa kuendelea kusababisha upepo wenye unyevu kiasi kuvuma kutoka kusini mashariki kuelekea katika ukanda wa pwani. Kwa upande mwingine joto la bahari la chini kidogo ya wastani Kusini-mashariki mwa Bahari ya Atlantiki linatarajiwa kuendelea. Hii inatarajiwa kuendelea kupunguza nguvu ya upepo wenye unyevu kutoka katika msitu wa Congo kuelekea katika maeneo ya magharibi na kusababisha kua

makavu.

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA SIKU KUMI (11 –20 SEPETEMBER, 2017)

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): Makavu kwa ujumla, vipindi vichache vya mvua zitakazoambatana na ngurumo katika Ziwa Victoria, na hali ya ubaridi vinatarajiwa.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): Makavu kwa ujumla, vipindi vichache vya mvua hususani katika maeneo ya miinuko na hali ya ubaridi vinatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Makavu kwa ujumla, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususani katika mkoa wa Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba. Hali ya ubaridi na upepo mkali katika ukanda wa mwambao vinatarajiwa

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Makavu kwa ujumla, hali ya ubaridi inatarajiwa,

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Makavu kwa ujumla na hali ya ubaridi inatarajiwa,

Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Njombe, Iringa na Mbeya): Makavu kwa ujumla, vipindi vichache vya mvua hususani katika maeneo ya miinuko na hali ya ubaridi vinatarajiwa.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Makavu kwa ujumla, vipindi vichache vya mvua. Hali ya ubaridi na upepo mkali katika ukanda wa mwambao vinatarajiwa

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma): Makavu kwa ujumla

Imetolewa na; **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**